# “Mihadarati na vileo – Poromoko la jamii”

## Episode 10 “Mwanzo mpya”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**PROOFREADER: Charlotte Collins**

**List of characters by scene:**

**<u>SCENE ONE: BERI'S NEW OFFICE</u>**

- **Inspekta Tino (m, 40)**
- **Beri (f, 45)**

**<u>SCENE TWO: JABALI'S PLACE</u>**

- **Chambo (m, 30)**
- **Zula (m, 18)**
- **Jabali (m, 18)**

**<u>SCENE THREE: LIMBI HIGH SCHOOL</u>**

- **Bi. Chacha (f, 45)**
- **3-5 Mixed voices (m/f 14-18)**

**SCENE FOUR: JABALI'S PLACE**

- **Chambo (m, 30)**
- **Zula (m, 18)**
- **Jabali (m, 18)**

**SCENE FIVE: MUGO'S OFFICE**

- **Chambo (m, 30)**
- **Mugo (m, 40)**

**Msimulizi (m/f)**

**INTRO:**

Hujambo na karibu katika kipindi cha Noa bongo! Jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha kumi na cha mwisho kwenye tamthilia hii iitwayo **“Poromoko la jamii”**, inayohusu utumiaji wa mihadarati na vileo Afrika. Katika kipindi kilichopita, waziri Kafegi alijiuzulu wadhfa wake baada ya kuhusishwa na kashfa ya kuingiza mihadarati nchini. Huku mwenzake, mheshimiwa Kizito akishikwa. Kwengineko, Chambo alikuja kazini akiwa mlevi, na kumuacha Jabali akijiuliza kama amerudia tena mihadarati. Maafisa Beri na Tino walipandishwa vyeo na kupelekwa kwenye kitengo cha askari wanaopambana na mihadarati. Leo tunatamatisha hadithi hii kwa kichwa **“Mwanzo mpya”.** Hebu kwanza, tukatane na Kamishna Beri pamoja na Inspekta Tino wakianza majukumu mapya kwenye ofisi yao mpya.

**SCENE ONE: BERI'S NEW OFFICE**

1. **SFX: SWIVEL CHAIR SWINGING FROM SIDE TO SIDE**

2. **INSP. TINO:** Bado umeduwazwa na afisi yako mpya, kiti kimekuwacha hoi?

3. **BERI:** Ninawaza, Tino.

4. **INSP. TINO:** Kuhusu nini, Bi. Kamishna?

5. **BERI:** Kuna ripoti katika meza yangu inayosema kuna kijana alipatikana amefariki, waliomuona ni marafiki zake na alikuwa amekula unga kiasi kikubwa.

6. **INSP. TINO:** **(annoyed)** Yote ni kazi ya Bamju! Yeye ndiye anayesambazia vijana madawa haya. Laiti hungelimuachilia wakati nilimshika… yasingelijiri haya…

7.

8. **BERI:** **(firmly)** Usinibwagie lawama, Inspekta! Nilikuwa nafuata amri za wakubwa– sikuwa na taarifa kuwa Bamju alikuwa na marafiki wenye mamlaka na ushawishi mkubwa serikalini ambao walimtoa. Lazima tuweke mikakati pamoja, Inspekta, iwapo tunataka kuondosha hii mihadarati katika mitaa yetu.

**9.** **INSP. TINO:** Nakubaliana nawe. Bi. Kamishna, lengo letu ni kuondosha mihadarati kabisa. Ijapokuwa haituhusu, lakini tutafanyaje kuhusu vileo vinavyokubaliwa kisheria? Kama pombe, mairungi, na tumbaku. Hizi ndizo kianzilishi cha madawa sugu kama heroini.

**10.** **BERI:** Kweli. Watu ni lazima waelimishwe kuwa kadri wanavyotumia madawa haya ndivyo wanavyozidi kudidimia katika lindi la mihadarati hii.

**11.** **INSP. TINO:** Unafikiria kweli tutafaulu kukomesha mihadarati?

**12.** **BERI:** Bila shaka! Lakini sharti tushirikiane na wengine. Tunahitaji msaada wa serikali, viongozi wa kidini, wazazi, waalimu na wafanyikazi wengine wa umma. Liwe jukumu la kila mtu.

**13.** **INSP. TINO:** kuna huyu kijana anaitwa Chambo…

**14.** **BERI:** Chambo wa Youth Watch? Huyu manusura wa mihadarati?

**15.** **INSP. TINO:** Haswa! Labda kitengo hiki chetu cha askari kingelifanya kazi pamoja na yeye. Anawajuwa watumizi, anawajuwa wauzaji, na bila shaka wauzaji watajuwa mihadarati hiyo inatoka wapi.

**16. BERI:** Ni wazo zuri. Nitafutie Chambo. Ni muhimu tupange kukutana naye.

**17. MSIMULIZI:** Beri hakuongopa: polisi peke yao katu hawatositisha mihadarati. Nchi inajukumu la kuweka sheria kali dhidi ya mihadarati – hususan inapokuwa inawahusu watoto. Wazazi na waalimu wana jukumu la kuwaelimisha watoto, kwa kuwapa mfano mwema, na mafunzo shuleni kuhusu maafa ya mihadarati hii. Lakini kwa sasa twende nyumbani kwa Jabali kule ambako Chambo tembo limeanza kumpunguka kichwani.

**SCENE TWO: JABALI'S PLACE**

| | | |
|---|---|---|
| 18. | **SFX: SOMEONE TAKING A SHOWER** | |
| 19. | **JABALI:** | **(calls out)** Wewe Zula, hebu toka huko bafuni! Umeingia yapata saa nzima sasa. |
| 20. | **ZULA:** | Ulitarajia nini? Nina mawiki sijaoga! Chambo anaendeleaje? |
| 21. | **JABALI:** | Ameanza kubumburuka. Ndio maana nataka utoke bafuni. |
| 22. | **SFX: SHOWER TURNED OFF; DOOR OPENED** | |
| 23. | **JABALI:** | **(surprised)** Lo! Umebadilika… kwa uzuri lakini… ijapokuwa bado hujasafishika itakikanavyo. |
| 24. | **CHAMBO:** | Vipi jamaa… Mbona niko hapa? Kwani kulitokea nini? |
| 25. | **JABALI:** | Chambo, hukumbuki tukikuleta hapa? |
| 26. | **ZULA:** | Atakumbuka vipi? Kalala njia yote. |
| 27. | **CHAMBO:** | Bafuni kuna mtu? |
| 28. | **JABALI:** | Hamna, lakini muhimu tuzungumze ukishamaliza. |

**29. SFX: DOOR CLOSED**

**30. MSIMULIZI:** Chambo akioga, kila dakika iliopita ilimpa kumbukumbu ya yale yaliyomtokea moja baada ya moja. Kulitokea nini hasa? Chambo aling’ang’ana kukumbuka… Punde tu, katika shule ya upili ya Limbi, Bi. Chacha alipata habari ya tanzia ya Okosho kufuatia utumizi wa mihadarati kwa kiwango kikubwa. Akaamua kuchukuwa hatua.

## SCENE THREE: LIMBI HIGH SCHOOL

**31. SFX: SCHOOL BELL RINGS**

**32. BI. CHACHA:** Leo ni siku ya huzuni sana hapa shuleni, kama wengine wenu mulivyopata habari. Tumempoteza mwanafunzi wetu wa kitambo kupitia njia ya uchungu sana. Okosho alipatikana tayari ameaga dunia na marafiki zake,baada ya utumizi mwingi wa heroini.

**33. SFX: SHOCKED EXCLAMATIONS AND SHOCKED REACTIONS FROM STUDENTS (studio)**

**34. BI. CHACHA:** Siku chache kabla, Zula na Okosho walinipora nikitoka benki. Sikufahamu walikua wanatumia mihadarati kwa wingi jinsi hio. Kijana wangu mwenyewe nimempeleka kituo cha kurekebisha tabia. Lakini najuwa wengine wenu mumeanza kutumia mihadarati.

**35. SFX: CHORUS OF DENIALS AND MURMURS FROM STUDENTS (studio)**

**36. BI. CHACHA:** Chaguo ni lenu. Mukane, au muchague kuishi maisha masafi bila mihadarati na vileo vyengine. Mimi na wenzangu tumekutana kwa dharura, na tumeona umuhimu wa kuwa na chama cha marika ili kuelimishana hapa shuleni.

**37. SFX: APPLAUSE FROM STUDENTS (studio)**

**38. BI. CHACHA:** Chama hiki kitafanya kazi kikishirikiana na Chambo na lengo ni kuwasaidia wale ambao tayari wanatumia madawa ya kulevya. Namaliza kwa kumnukuu Chambo alivyosema awali: Tafadhali wacha madawa kabla hayaja kunasa! Sawa – munaweza kurudi darasani.

**39. MSIMULIZI:** Huku wanafunzi wakirudi madarasani, Chambo sasa alifahamu kila kitu kilivyotokea, na ni kwanini Jabali alimpata katika hali ile. Ukweli ulimshangaza zaidi Jabali kuliko vile alivyofikiria.

## SCENE FOUR: JABALI'S PLACE

| | | |
|---|---|---|
| **40.** | **JABALI:** | **(shocked)** Hapana! Sisadiki! Una hakika, Chambo? |
| **41.** | **CHAMBO:** | Hakika kama mauti! Niliwekewa madawa ya kulevya. Mtu aliniwekea katika kinywaji changu kule kilabu 2000. Sasa ndiyo nafahamu ilivyotokea. |
| **42.** | **ZULA:** | **(still with a nervous voice because of his addiction)** Unajuwa, Sishangai. Nishasikia wanawake wengi hujipata uchi baada ya kuwekewa vileo kwenye vinywaji katika majumba ya muziki na migahawa. |
| **43.** | **CHAMBO:** | Labda walitaka kunitisha . Mlinzi aliniambia tangu nianze kuchunguza vitambulisho vya watu, biashara imekwenda chini . |
| **44.** | **JABALI:** | Siamini! Walikuibia chochote? |
| **45.** | **CHAMBO:** | La, Lengo lao ni kunitishia au kuniregesha kwenye mihadarati. |
| **46.** | **ZULA:** | Na hivyo ndivyo mimi na Jabali tulifikiria. |

**47. CHAMBO:** Ati? Kwamba nimerudia ulevi? Hapana. Hayo nimemalizana, rafiki yangu, na siwezi kurudia maisha hayo.

**48. JABALI:** Unamkumbuka Okosho? Yule rafiki yangu mwengine?

**49. ZULA:** Yule alitimuliwa kilabu 2000. Unamjuwa, Yule hata alijaribu kupigana na wewe.

**50. CHAMBO:** **(ANAKUMBUKA)** Aaah, yule. Bila shaka ninamfahamu. Alikuwa mlevi sana, kisha mshari. Alinikumbusha sana maisha yangu ya kale, nilipokuwa natumia madawa.

**51. JABALI:** Okosho alifariki.

**52. CHAMBO:** **(shocked)** Ati? Lini ? Vipi? Poleni sana.

**53. JABALI:** Unakumbuka tulipoona umati unapiga mtu fulani…

**54. CHAMBO:** **(more shock)** Usiniambie ni yeye ndiye alikuwa anapigwa. Usiniambie umati ulimuua.

**55. ZULA:** La, mwizi aliyekuwa akipigwa si Okosho. Ni mimi.

**56. CHAMBO:** Hebu – sasa mnanichanganya.

**57. JABALI:** Najuwa. Nitakueleza, lakini kwa sasa tuna kazi ya kufanya. Pia nina habari njema za kukupa , kuna watu wanataka kukupa msaada wa kufanya kazi katika kituo cha kubadili tabia.

**58. CHAMBO:** Ah! Hizo ni habari njema.

**59. ZULA:** Kabla hatujaondoka, nina machache. Nimepoteza rafiki, mimi mwenyewe karibu nife, na nimeona jinsi madawa yalivyoniathiri. Nashindwa nitaacha vipi. Lakini niko tayari kwenda katika kituo cha kubadili tabia. Haitakuwa rahisi lakini ni tayari kuanza upya.

**60. JABALI:** Zula – leo najivunia kuwa rafiki yako.

**61. CHAMBO:** Zula, umeamuwa vyema. Sasa – unafikiri nini, Jabali? Tuanzie wapi?

**62. ZULA:** Kilabu 2000? **(They all laugh heartily)**

**63. MSIMULIZI:** Zula amechukuwa hatua moja lakini muhimu sana**.** Ni vigumu sana kwa muathirika kukubali kuwa yeye ni muathirika. Wengi hawasadiki kama kina Okosho mpaka yawatie kaburini. Lakini kwa wale wanaotaka kuanza upya, hakuna lisilowezekana. Siku hiyo hiyo, baada ya kumpeleka Zula kituo cha kubadili tabia, Chambo alimtuma Jabali kufanya kazi zake wakati yeye akimtembelea Mugo afisini mwake kwa mahojiano ya faragha gazetini.

**SCENE FIVE: AFISI YA MUGO**

**64. MUGO:** Karibu “The Voice”, Bw. Chambo. Mimi ni mvutaji sigara. Hiyo ni mihadarati?

**65. CHAMBO:** Bw. Mugo. Sitojali ukivuta sigara. Tatizo ni ukishindwa kujizuia hamu hiyo ya uvutaji sigara.

**66. MUGO:** Hmm… unanifurahisha. Basi wacha nijitayarishe tuanze.

**67. SFX: PAPER FLIPPING; PEN SCRIBBLING ON PAPER (studio)**

**68. CHAMBO:** Naweza kukuuliza swali, Bw. Mugo?

**69. MUGO:** Nilifikiri ni mimi wakukuuliza. **(laughs)** Ni utani. Endelea, ni utani.

**70. CHAMBO:** Unathamini maisha yako?

**71. MUGO:** Zaidi ya kitu chochote.

**72. CHAMBO:** Unajua kusoma, Bw. Mugo?

**73. MUGO:** **(bewildered)** Ati? Bila shaka. Mimi ni mwanahabari!

**74. CHAMBO:** Vizuri! Hebu soma haya maelezo yaliyoandikwa kwenye pakiti hii ya sigara.

| | | |
|---|---|---|
| **75.** | **MUGO:** | **(sighs)** Sidhani kama nitawacha sigara kwa vitisho kama hivi? |
| **76.** | **CHAMBO:** | Soma kwanza, alafu tuendelee. |
| **77.** | **MUGO:** | **(takes a deep breath, then reads in a bored voice)** *Uvutaji wa sigara unadhuru afya yako*. Enhe – kwa hivyo? |
| **78.** | **CHAMBO:** | Kwa hivyo? Ni sehemu ipi ya sentesi hiyo ambayo hukuelewa? Bw. Mugo, unafahamu kuwa sigara unayovuta ina zaidi ya kemikali 4.000 tofauti? Mbali na nikotini, inayokupa hamu ya kuvuta sigara hiyo, kuna kemikali kama *carbon monoxide*, *methanol,* na nyengine nyingi. |
| **79.** | **MUGO:** | Hmm. Sasa umeanza kunitisha. Sikuwa najuwa. **(Pause)** kemikali 4,000? Kweli? |
| **80.** | **CHAMBO:** | Ndio, ukweli mtupu. Lakini tutazungumzia hayo hivi punde. Tunaweza kuanza mahojiano? |

**OUTRO:**

Chambo alimueleza Bw. Mugo kemikali zote zilizo katika mihadarati mbali mbali, na madhara yake katika mwili, tumbaku na hata gamu ya viatu inayonuswa na chokoraa mitaani. Alizungumzia kazi kuhusu kazi yake, na jinzi angelipenda kuona kizazi kinachoishi bila utumiaji wa mihadarati. Akamtaja Jabali, Zula na kifo cha Okosho. Vita dhidi ya mihadarati vimeanza kupamba moto. Wanasiasa fisadi wanatupwa gerezani, na tangu kashfa hii ianze na biashara ya madawa kuvurugwa Bamju alipotea. Bila shaka, Kamishna Beri, Inspekta Tino, Chambo, Bi. Chacha, Jabali na wengineo wakishirikiana, basi ushindi utapatikana.

Hapa ndipo tunatia nanga tamthilia hii inayohusu mihadarati na vileo. Ni tumaini letu kuwa umeburudika na kujifunza. Mwandishi alikua Chrispin Mwakideu. Ukipenda kusikiliza vipindi vyote vilivyotangulia utavipata katika tovuti yetu www.dw.de/lbe.Hadi wakati mwengine, kwaheri na jiepushe na madawa ya kulevya!